CHUO CHA USTAWI WA JAMII

DAR ES SALAAM & KILIMANJARO



# JARIDA LA MTANDAONI

JULAI - SEPTEMBA, 2025



Mkuu wa Chuo Dkt. Joyce Nyoni akihotubia katika hafla ya makabidhiano ya uongozi wa serikali ya wanafunzi ISWOSO

# MAKABIDHIANO YA UONGOZI SERIKALI ZA WANAFUNZI (ISWOSO) 2024/2025 – 2025/2026

serikali ya wanafunzi (ISWOSO) ya mwaka wa masomo 2024/25 ilikabidhi rasmi majukumu na madaraka kwa serikali mpya ya wanafunzi ya mwaka 2025/26 katika hafla ya makabidhiano iliyofanyika tarehe 4 Julai 2025, Dar es Salaam, tukio lililoongozwa na Menejimenti ya Chuo cha Ustawi wa Jamii.

Mgeni rasmi katika hafla hiyo, Mkuu wa Chuo, Dkt. Joyce Nyoni, aliwapongeza viongozi wa awali kwa mchango wao na kufanikisha maendeleo ya wanafunzi, huku akiwasisitiza viongozi wapya kuzingatia maadili, uwajibikaji, uwazi, na kutanguliza mbele maslahi ya wanafunzi waliowaamini kwa kuwachagua. Dkt. Joyce Nyoni pia aliwakumbusha kuwa jukumu la msingi la kila mwanafunzi ni kusoma kwa bidii, kushirikiana kwa uwazi, na kutumia fursa zote za kielimu na kiutendaji ili kutimiza malengo makubwa ya kitaaluma. Hafla hiyo iliashiria utamaduni wa kuendeleza uongozi bora miongoni mwa wanafunzi.



Mkuu wa Chuo Dkt. Joyce Nyoni akikabidhi cheti cha pongezi kwa Abdallah Zidane - rais wa ISWOSO 2025/2026



Mkuu wa Chuo Dkt. Joyce Nyoni akikabidhi cheti cha pongezi kwa Method Dallu - rais wa ISWOSO 2024/2025



Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Wakili Amon Mpanju (kushoto) akiteta jambo na Mkuu wa Chuo, Dkt. Joyce Nyoni (kulia) walipotembelea banda la ISW katika Maonesho ya 49 ya Sabasaba.

# USHAURI WA KITAALUMA NA KISAIKOLOJIA WATOLEWA NA CHUO CHA USTAWI WA JAMII KATIKA MAONESHO YA 49 YA SABASABA

Chuo cha Ustawi wa Jamii ni miongoni mwa vyuo vya elimu ya juu ambavyo vilitoa huduma kwa wananchi wa mkoa wa Dar es Salaam katika Maonesho ya 49 ya Biashara ya Kimataifa (Sabasaba) ambayo yalianza tarehe 28 Juni - 13 Julai, 2025 katika Uwanja wa Maonesho wa Mwalimu Julius K. Nyerere, jijini Dar es Salaam.

Katika maonesho hayo, Chuo cha Ustawi wa Jamii kilitoa huduma mbalimbali kwa wananchi waliotembelea banda hilo. Huduma zilizotolewa wakati wa maonesho hayo ni, ushauri na msaada ya kisaikolojia, ushauri wa kitaaluma na maelezo kuhusu huduma zinazotolewa na Chuo cha Ustawi wa Jamii katika kampasi kuu ya Kijitonyama, Dar es salaam pamoja na kampasi ya Kisangara, Mwanga iliyopo mkoani Kilimanjaro. Huduma za udahili kwa mwaka wa masomo 2025/2026 pia zilitolewa katika maonesho hayo.



Mhadhiri Msaidizi Asteria Mlambo (katikati) akielezea huduma zinazotolewa na Chuo kwa wananchi waliotembelea banda la Chuo katika Maonesho ya 49 ya Sabasaba yaliyofanyika jijini Dar es Salaam.


Mhadhiri Msaidizi Amina Abdallah (kushoto) akitoa huduma ya msaada wa kisaikolojia kwa mwananchi alietembelea banda la Chuo katika Maonesho ya 49 ya Sabasaba yaliyofanyika jijini Dar es Salaam.




Mhadhiri Msaidizi Lucy Michael katika picha ya pamoja na Wanafunzi waliotembelea banda la Chuo cha Ustawi wa Jamii katika Maonesho ya Sita ya Elimu ya Juu yaliyofanyika Zanzibar.

# ISW YASHIRIKI MAONESHO YA SITA YA ELIMU YA JUU ZANZIBAR 2025

Chuo cha Ustawi wa Jamii kilishiriki kikamilifu katika Maonesho ya Sita ya Elimu ya Juu Zanzibar yaliyofanyika kuanzia tarehe 14 Julai hadi 20 Julai 2025 katika Viwanja vya Mnazi Mmoja, Unguja, Zanzibar.

Wageni waliotembelea banda la chuo walipata huduma mbalimbali, ikiwemo huduma za udahili kwa mwaka wa masomo 2025/2026, ushauri wa kitaaluma, msaada wa kisaikolojia maelezo kuhusu programu zinazotolewa katika kampasi kuu ya Kijitonyama, Dar es Salaam, pamoja na kampasi ya Kisangara, Mwanga mkoani Kilimanjaro.

Maonesho hayo yameimarisha uhusiano kati ya Chuo na jamii na kuwezesha jamii kupata ufahamu mzuri kuhusu mchango wa Chuo cha Ustawi wa Jamii katika kukuza maendeleo endelevu katika jamii.



Mhadhiri Msaidizi Rufina Khumbe (kushoto) akielezea huduma zinazotolewa na Chuo kwa wananchi waliotembelea banda la Chuo katika Maonesho ya Elimu ya Juu yaliyofanyika Zanzibar.

# WATAALAM WA USTAWI WA JAMII KUTAFUTA SULUHISHO ENDELEVU KWA WATOTO WA MITAANI

**Tarehe 17 Julai 2025, Wataalam wa Ustawi wa Jamii kutoka Chuo cha Ustawi wa Jamii, wakishirikiana na Uongozi wa Kata ya Ubungo, wadau maendeleo walikusanyika katika Ofisi za Kata ya Ubungo kwa kikao maalum kilicholenga kujadili afua bora za kusaidia watoto wanaoishi na kufanya kazi mitaani.**



Mhadhiri Msaidizi Juliana Mheluka (Kushoto) akiwasilisha mjadala kuhusiana na afua bora za kusaidia watoto wanaoishi na kufanya kazi mitaani katika kikao na wadau wa maendeleo.

**Kikao hiki kililenga kuishirikisha jamii kwa pamoja ili kutatua changamoto zinazowakabili watoto hao, kupata ushirikiano kutoka kwa wananchi, na kusikiliza maoni pamoja na mapendekezo ya wazazi, walimu, na wadau wengine kuhusu njia bora za kuwasaidia watoto wa mitaani. Mjadala ulijikita katika njia za malezi, upatikanaji wa elimu, na msaada wa kijamii unaoweza kubadilisha maisha ya watoto hao. Aidha, kikao kilijadili mbinu za kutambua watoto wanaohitaji msaada wa haraka na namna ya kuhakikisha kila mtoto anapata ulinzi, malezi bora, na elimu.**



Wadau wa maendeleo wakisikiliza mawasilisho juu ya mjadala kuhusu afua bora za kusaidia watoto wanaoishi na kufanya kazi mitaani.



Mwanafunzi wa ISW akimuuliza swali Msimamizi wa Kiwanda cha Kiboko kuhusiana na shughuli za uendeshaji.

## WANAFUNZI WA ISW WAJIFUNZA AFYA NA USALAMA MAHALA PA KAZI KATIKA KIWANDA CHA KIBOKO

Wanafunzi wa Chuo cha Ustawi wa Jamii tarehe 24 Julai 2025, walitembelea kiwanda cha Kiboko Continuous Galvanizing Line kilichopo Mikocheni, Dar es Salaam, kwa ziara ya kitaaluma iliyoandaliwa kwa lengo la kuunganisha elimu ya darasani na uzoefu wa vitendo.

Ziara hii iliwawezesha wanafunzi kupata uelewa wa moja kwa moja kuhusu mahitaji ya afya na usalama kazini, mchakato wa uzalishaji, na changamoto zinazoweza kutokea mahala pa kazi. Wanafunzi waliona kwa karibu hatua za kiutendaji zinazofuatwa kuhakikisha usalama wa wafanyakazi, matumizi ya vifaa vya kinga, na masharti ya kuepuka ajali kazini.

Mbali na kupokea mafunzo ya vitendo, wanafunzi walipata fursa ya kuuliza maswali na kupata maelezo kutoka kwa wasimamizi wa kiwanda, jambo lililowawezesha kuelewa uhalisia wa yale wanayojifunza darasani na kuunganisha nadharia.



Wanafunzi wa ISW wakipokea maelezo kutoka kwa msimamizi wa kiwanda kuhusiana na shughuli za uendeshaji.



Picha ya kiwanda cha Kiboko Continous Galvanizing line kinachojihusisha na utengenezaji wa mabati.

# ISW YASHIRIKI MAONESHO YA KILIMO NANENANE

Chuo cha Ustawi wa Jamii kilishiriki kikamilifu Maonesho ya Kilimo Nanenane yaliyofanyika kwenye Viwanja vya Nzuguni, Dodoma kuanzia tarehe 1 hadi 10 Agosti 2025. Ushiriki wa Chuo katika maonesho hayo ililenga katika kutoa huduma, elimu, na mwongozo kwa wananchi waliotembelea banda la chuo, huku likionyesha jinsi elimu inayotolewa katika Chuo cha Ustawi wa Jamii inaweza kuunganishwa na maendeleo ya jamii.



Mhadhiri Msaidizi Salama Rajabu (kushoto) akimuonesha Katibu Mkuu (WMJJWMM) Dkt. John Jingu (kulia) chumba maalum kilichoandaliwa kwajili ya kutoa ushauri na msaada wa kisaikolojia kwa wageni watakao tembelea banda la Chuo katika Maonesho ya Nanenane, Dodoma.




Mhadhiri Msaidizi Abubakar Fadhili (kushoto) akimuonesha Mkuu wa Chuo Dkt. Joyce Nyoni (kulia) vifaa vinavyotumika kuleta uchangamshi wa awali kwa mtoto vilivyopo kwenye banda la Chuo katika Maonesho ya Nanenane, Dodoma.

Wageni walipata fursa ya kupata huduma za udahili kwa mwaka wa masomo 2025/2026, kupata ushauri wa kitaaluma, na pia kupata msaada wa kisaikolojia. Zaidi ya hayo, walipewa maelezo kuhusu programu zinazotolewa katika kampasi kuu ya Kijitonyama, Dar es Salaam, pamoja na kampasi ya Kisangara, Mwanga mkoani Kilimanjaro.




Afisa Mitihani Kabongo Reid (mwenye t-shirt ya kijivu) na Mhadhiri Msaidizi Abubakari Fadhil (mwenye t-shirt ya bluu bahari) wakizungumza na mgeni aliyetembelea banda la Chuo katika Maonesho ya Nanenane yaliyofanyika Dodoma.

# MAADHIMISHO YA WIKI YA USTAWI WA JAMII 2025 YAFANYIKA KITAIFA DAR ES SALAAM

**Tanzania iliadhimisha Wiki ya Ustawi wa Jamii kitaifa kwa mara nyingine, ambapo maadhimisho ya mwaka huu yalifanyika katika Viwanja vya Chuo cha Ustawi wa Jamii, Kijitonyama – Dar es Salaam kuanzia tarehe 25 hadi 30 Agosti 2025.**



Mratibu wa Kituo cha Elimu, Ushauri na Msaada wa Kisaikolojia, Rufina Khumbe (kulia) akitoa maelezo kwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Mhe. Dkt. Dorothy Gwajima (kushoto) alipotembelea banda la ISW katika Maonesho ya Wiki ya Ustawi wa Jamii 2025.

**Maadhimisho hayo yalibeba kauli mbiu isemayo: “Pata Msaada wa Kisaikolojia; Imarisha Afya ya Akili”, ikilenga kutoa elimu kwa jamii kuhusu umuhimu wa huduma za kijamii na kisaikolojia katika kuimarisha ustawi wa watu binafsi, familia na taifa kwa ujumla. Maadhimisho hayo yaliambatana na maonesho ambapo wananchi walipata wasaha wa kutembelea banda la chuo na kupata huduma mbalimbali ikiwemo ushauri na msaada wa kisaikolojia, elimu kuhusu malezi ya watoto, ushauri wa kitaaluma, pamoja na huduma za udahili kwa mwaka wa masomo 2025/2026.**



Mratibu wa Kituo cha Elimu, Ushauri na Msaada wa Kisaikolojia, Rufina Khumbe (kulia) akitoa maelezo kwa Katibu Mkuu wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Mhe. Dkt. John Jingu (kushoto) alipotembelea banda la ISW katika Maonesho ya Wiki ya Ustawi wa Jamii 2025.

# KURASA RASMI ZA CHUO CHA USTAWI WA JAMII

**INSTAGRAM**

ISW_OFFICIAL_TZ

**TWITTER (X)**

TAASISIYAUSTAWI

**WHATSAPP CHANNEL**

CHUO CHA USTAWI WA JAMII

**YOUTUBE CHANNEL**

CHUOCHAUSTAWIWAJAMII

TAASISI YA USTAWI WA JAMII

HUDUMA HUKUZA MAENDELEO

# CHUO CHA USTAWI WA JAMII


210 Shekilango Road

P.O. BOX 3375

14113 Kijitonyama

Dar es Salaam

+255735509090

+255677111200

+255716121096

or

info@isw.ac.tz